18. Kiasi cha akiba kinachoweza kulipika kwa mwanachama wa Mfuko kwa madhumuni ya vifungu vya 32, 33 na 36 vya Sheria hii kitakuwa ni sawa na jumla ya makusanyo ya michango yote iliyofanywa kwa ajili ya mwanachama huyo, toa makusanyo yanayoainishwa katika ibara (a) ya kijifungu cha (2) cha kifungu cha 19 na mikato yote inayofanywa chini ya kijifungu cha (3) cha kifungu hicho, na kwa kuzingatia maelezo ya kijifungu cha (3) cha kifungu cha 19, kiasi cha riba ambacho kitaweza kuwa kimelipwa kwa mwanachama huyo chini ya masharti ya kijifungu hicho kilichotajwa.

SEHEMU YA TANO

UWEKAJI WA MALIPO KATIKA MFUKO.

Michango kulipwa
kwenye mfuko na
lugaiwa kwa
wanachama.

19. (1) Kima chote kilichopokelewa au kukusanywa kwenye akaunti ya michango chini ya masharti ya Sheria hii yatalipwa au yatahamishiwa kwenye Mfuko kama Bodi itavyoelekeza.

(2) Kiasi cha fedha kitachowajibika kulipwa kwenye Mfuko chini ya masharti ya vifungu vya 14,

17 na 24 vya Sheria hii vitalipwa kama ifuatavyo -

- (a) sehemu moja katika saba ya kima kwenye kasma ya mapato ya jumla ya Mfuko kwa ajili ya kufanya malipo ya miaka chini ya matoleo yatayofanywa chini ya masharti ya Ibara (b) ya kifungu cha 68 cha Sheria hii; na
- (b) sehemu sita katika saba ya kima kwenye akaunti ya mwanachama ambae zimelipwa kwa ajili yake.
- (3) Bodi itahakikishe fedha zinalipwa kwenye akaunti ya kila mwanachama wa Mfuko kwa vima vinavyolingana na masharti yaliyowekwa chini ya ibara (b) ya kifungu cha (2) cha kifungu hiki, katika kila kipindi cha mwaka wa fedha kwa ajili ya mwanachama huyo, na kufuatia uamuzi wa Bodi chini ya masharti ya kifungu cha 9, juu ya kiwango cha riba cha mwaka wa fedha unachusika, riba kwa kiasi anachostahiki kulipwa wakati wa kuanza mwaka huo katika hali ambayo Bodi itaelekeza na kukata shilingi ishirini kutoka kwenye akaunti ya kila mwanachama au, ikiwa kiasi kinachostahiki kulipwa kwa mwanachama huyo kitakuwa chini ya shilingi ishirini, kiasi hicho kitaendelea kwenye mapato ya jumla ya Mfuko.

Isipokuwa kwamba ikiwa maombi hayo hayakufanywa mpaka zaidi ya miezi sita baada ya tarehe ambayo amefika umri wa kustaafu, mchango utaendelea kulipwa kwa ajili yake na hataruhusika kuacha mpaka atakapotoa taarifa ya miezi sita kwamba anajitoa, au kipindi kifupi zaidi ya hicho kama Bodi itavyoweza kukubali kwa mujibu wa kila kadhia.

(4) Mkataba wowote au makubaliano yatayoeleza kwamba mtu yoyote hatatoa taarifa kama ilivyoelezwa kwenye masharti ya kifungu cha (1) cha kifungu hiki yatakuwa batili na mkataba wowote au makubaliano yanayoeleza kwamba mtu yeyote atapeleka maombi ya kujitoa kwenye Mfuko kwa kima chochote cha akiha yake au baada ya kufikia umri wa kustaafu yatakuwa batili.

mapato mengine
asiyotokana
mchango.

20. Bodi baada ya kupata idhini ya Waziri inaweza kuweka vitega uchumi au kuanzisha vyanzo vyengine vya mapato ya Mfuko ambayo yatajumuishwa katika mapato ya jumla ya Mfuko.

SEHEMU YA SITA

WAZEE WALIOAJIRIWA TENA BAADA YA KUFIKIA UMRI
WA KUSTAAFU AU KUJITOA.

muajiriwa tena
na kuendelea
muajiriwa baada
ya kufikia umri
na kustaafu.

21. Waziri kwa kushauriana na Bodi anaweza kuweka kanuni chini ya Sheria hii na kutayarisha mpango wa kuwaingiza katika Mfuko wazee walioajiriwa tena baada ya kufikia umri wa kustaafu au baada ya kujitoa katika Mfuko.

SEHEMU YA SABA:

MIFUKO ILIYORUHUSIWA NA KURUHUSIKA.

likubaliwa
kwa mifuko
iliyoruhusiwa.

22. (1) Ikiwa Bodi itaridhika kwamba muajiri yeyote kabla ya siku ya mwanzo ya mwezi wa Julai, 1990 ameanzisha mfuko wa akiba au mfuko mwengine ambao unatoa kwa muajiriwa wake manufaa kifedha sio chini ya thamani ya manufaa yanayotolewa chini ya Sheria hii (ambao baadae katika Sheria hii, utajulikana kama mfuko ulioruhusiwa) Bodi itaathibitisha mfuko huo na kuanzia hapo muajiri huyo hatohusika na kuchangia kwenye Mfuko chini ya masharti ya kijifungu cha (1) cha kifungu cha 14, kwa ajili ya uajiri wa muajiriwa huyo ambao ni mwanachama wa mfuko huo ulioruhusiwa, kwa kadri ambavyo muajiri atachangia kwenye mfuko ulioruhusiwa kwa ajili ya muajiriwa kwa mujibu wa kanuni na taratibu za mfuko huo.

Isipokuwakwamba, Bodi haitathibitisha mfuko wowote ambao una masharti yanayoeleza kwamba mchangiji ataweza, katika hali yoyote, na kwa uamuzi wake kuchukua sehemu yoyote ya michango yake kwa mfuko huo au riba yoyote iliyochumwa au sehemu kubwa zaidi ya msaada wa muajiri ikilinganishwa na tofauti baina ya kima cha msaada huo na kima cha nusu moja ya

kiwango ambacho kingelipwa kwenye Mfuko kwa ajili yake chini ya masharti ya Sheria hii kwa kipindi cha uwanachama wake kwa Mfuko kama angekuwa mwanachama, tokea kuanza kutumika kwa Sheria hii.

(2) Muajiri yeyote ambae atataka kuiomba Bodi ithibitisha mfuko au mpango kuwa ni mfuko ulioruhusiwa chini ya masharti ya kijifungu (1) cha kifungu hiki atawasilisha maombi kupitia utaratibu uliowekwa, kwenye Bodi, ndani ya kipindi cha miezi sita tokea kuanza kutumika kwa sheria hii, na iwapo Bodi itaridhika kwamba maombi hayo ni sawa itatoa shahada ya muda ya kumruhusu muajiri kutoka kwenye masharti ya sheria hii kuhusiana na wanachama wa mfuko huo mpaka hapo Bodi itapoamua kuridhika au kutoridhika kwamba mfuko huo umekubaliwa, na endapo Bodi haitaridhika itamjulisha muajiri na hapo masharti ya sheria hii yatatumika kikamilifu.

Isipokuwa kwamba, bila ya kujali masharti ya kijifungu cha (1) cha kifungu cha 14 cha Sheria hii hakuna mchango utakaolipwa kwenye Mfuko katika mwezi ambao Bodi itamjulisha hivyo muajiri.

Ubatilishaji wa ruhusa.

23. Iwapo katika wakati wowote maslahi yaliyotolewa na muajiri chini ya mfuko uliokubaliwa, kwa maoni ya Bodi yamesita kuwa bora (zaidi) kuliko yale ya Mfuko wa Akiba, au iwapo Bodi hairidhishwi na uongozi wa mfuko wowote uliokubaliwa, basi Bodi itaweza kubatilisha shahada yoyote iliyotolewa kwa mujibu wa kijifungu cha (1) cha kifungu cha 22 cha Sheria hii, na hapo maelezo ya vifungu vya 24 na 27 vya Sheria hii yatatumika kama vile ambavyo yangetumika kama mfuko huo umefungwa.

Thaulishaji wa akiba kuingia kwenye Mfuko.

24. (1) Muajiriwa yeyote ambae hajafikia umri wa kustaafu na akaacha uajiri ambao kwao alikuwa ni mwanachama wa mfuko ulioruhusiwa au akasita kuwa na michango iliyolipwa kwenye mfuko huo kwa ajili yake kwa sababu nyengine yoyote ukiondoa ya kifo chake, muajiri anaehusika atalipa kwenye Mfuko ama -

- (a) kiasi cha fedha ambacho kingekuwa kimelipwa kwenye Mfuko kwa ajili ya muajiriwa huyo kama yangefuatwa masharti ya Sheria hii, kwa kipindi cha uanachama wake katika mfuko huo ulioruhusiwa tokea kuanza kutumi-ka kwa sheria hii jumlisha na riba ambayo ingelipwa kwa muajiriwa huyo kama ambapo michango hiyo ingelipwa chini ya sheria hii; au
- (b) nusu ya kima hiki jumlisha na kiasi cha akiba cha muajiriwa huyo katika mfuko ulioruhusiwa ambacho kinawakilisha mchango wa muajiriwa huyo tokea kuanza kwa Sheria hii, pamoja na riba iliyochumwa.

katika hivyo viwili kitachokua kikubwa zaidi ndicho kitachochukuliwa. Malipo hayo yatafanywa ndani ya kipindi cha mwezi mmoja tokea muajiriwa anaposita kuwa mwanachama wa mfuko huo ulioruhusiwa, au ndani ya kipindi chochote cha ziada kitachoruhusiwa na Bodi kwa minterafu ya kila kadhia.

(2) Hakuna chochote katika kifungu cha (1) cha kifungu hiki kitachozuia kuhaulishwa kwenye Mfuko, katika hali ambayo kifungu kingeruhusu uhaulishaji wa kiasi chochote kuingia kwenye Mfuko, kwa makubaliano baina ya muajiri na muajiriwa, kiasi chochote cha akiba pamoja na riba ya muajiriwa huyo kilichomo kwenye mfuko ulioruhusiwa, kinachohitaji kuhaulishwa chini ya masharti ya kifungu hiki, au kiasi chochote kilichochangiwa kwenye mfuko huo kabla ya kuanza Sheria hii, pamoja na riba iliyochumwa.

(3) Pale ambapo muajiriwa aliyeajiriwa na muajiri mwenye mfuko ulioruhusiwa anapata uhamisho wa kikazi kutoka Zanzibar kwenda nje ya Zanzibar chini ya muajiri huyo huyo, haitochukuliwa kwamba muajiriwa huyo amesita kuchangia mfuko ulioruhusiwa.

malipo
alioruhusiwa.

25. (1) Pale ambapo kanuni na taratibu za mfuko wowote ulioruhusiwa zinaruhusu muajiriwa yeyote kuacha huduma za akiba ya uzeeni za muajiri ambae ameanzisha mfuko kama huo, kwa sababu ya kujiunga na bima ya maisha yake ambayo ameipata kwa kuinunua kwa michango yake mwenyewe au kwa michango ya muajiri wake kwenye mfuko huo, muajiriwa huyo anaweza kwa kutoa taarifa ya siku kumi na nne kwa muajiri wake na kwa Bodi kuelezea nia yake ya kuacha huduma hizo kama ilivyoelezwa, kujiunga na bima hiyo na bila ya kujali masharti yoyote ya bima hiyo, atajaaliwa kuwa ni mtu ambae maisha yake yamekatiwa bima.

(2)(a) Kiasi kitacholipwa kwa Bodi na muajiri chini ya masharti ya kifungu cha 24 cha sheria hii kitapungua kwa kadri ya kima cha fedha taslim kitachopokelewa na muajiriwa kuto-kana na bima chini ya masharti ya kijifungu cha (1) cha kifungu hiki.

(b) Kwa madhumuni ya kuhesabu thamani iliyoelezwa kwenye ibara ya (a) ya kijifungu hiki, muajiriwa kwa kila mwaka atawasilisha kwa kila mwanachama wa mfuko ulioruhusiwa na kwa Bodi, maelezo kuhusu bima inayoendelea ya mwanachama huyo kama Bodi itavyochitaji.

(3) Bila ya kujali masharti ya sheria nyengine yoyote au masharti ya bima yeyote, hakuna bima itakayopokelewa na mtu yeyote kuhusiana na masharti ya kijifungu (1) cha kifungu hiki itayogaiwa, wekwa amana, hamishwa au salimishwa kabla ya tarehe yake ya kustahiki malipo.

Uhaulishaji wa
akiba kwenye
mfuko
ulioruhusiwa.

26. Pale ambapo muajiriwa aliyemo katika ajira iliyoanzishwa mfuko ulioruhusiwa anazuilika kwa mujibu wa kanuni za mfuko huo kuchangia kwa kipindi kilichoainishwa cha majaribio kisichozidi mwaka mmoja, kiasi chochote kitathokua katika akaunti ya muajiriwa huyo katika Mfuko kitachotokana na

michango aliyolipiwa katika Mfuko kwa kipindi chote cha majaribio pamoja na riba iliyochunwa na kiasi hicho, kitahaulishwa kwenye akaunti yake ya mfuko huo ulioruhusiwa kama muajiriwa huyo atakuwa mwana-chama kamili wa mfuko huo baada ya muda wa majaribio kumalizima na kama kanuni za mfuko huo zinaruhusu hivyo.

fungwa kwa mfuko ulioruhusiwa.

26. Bila ya kujali masharti ya kifungu cha 24 cha Sheria hii, pale mfuko ulioruhusiwa unapofungwa Badi inaweza, ikiwa itaona kwamba ni muafaka kwa manufaa ya wajaariwa kufanya hivyo, kukubali mali na dhima za mfuko huo katika tarehe kama itavyokubalika na itaweza kuweka katika Mfuko akiba ya kila mwanachama wa mfuko huo uliofungwa, kiasi sawa na sehemu sita kati ya saba ya akiba yake atayokuwanayo kwenye mfuko ulioruhusiwa katika tarehe hiyo.

tarehe ya kopea fedha ulioruhusiwa na Bodi.

28. Michango iliyolipwa kwenye mfuko ulioruhusiwa haitajaaliwa kwa madhumuni yoyote kuhusiana na sheria hii kuwa imelipwa kwenye Mfuko kwa tarehe yoyote zaidi ya ile ambayo chini ya masharti ama ya kifungu cha 24 au cha 27 cha sheria hii itakua imepokelewa na Mfuko.

kanuni na Hesabu ya fedha za mfuko ulioruhusiwa.

29. Muajiri yeyote ambae ameanzisha mfuko ulioruhusiwa -

- (a) ataipatia Bodi taarifa za hesabu za fedha za mfuko huo, zikiwa zimethibitishwa na mhasibu aliyekubaliwa na Bodi, kama Bodi itavyohitaji;
- (b) atazifuata kanuni za mfuko huo ulioruhusiwa na atalipa michango na misaada kwenye mfuko huo ndani ya kipindi ambacho kanuni za mfuko huo zitahitaji;
- (c) ataiarifu Bodi juu ya mapendekezo yoyote ya marekebisho ya kanuni za mfuko ulio-

ruhusiwa na hatotekeleza marekebisho yoyote kati ya hayo isipokuwa kwa hati ya maandishi ya idhini itayotolewa na Bodi;

- (d) itaipatia Bodi marejesho yote kama Bodi itavyoeleza kuhusiana na waajiriwa ambao ni wanachama, au ambae wameacha kuchangia kwenye mfuko huo ulioruhusiwa.

Misamaha.

30. Iwapo Bodi, baada ya kuombwa na muajiriwa pamoja na muajiri wake, itaridhika kwamba -

- (a) muajiriwa ameajiriwa na muajiri ambaye afisi yake kuu iliyosajiliwa ipo nje ya Zanzibar chini ya mkataba wa uajiri uliofanywa nje ya Zanzibar;
- (b) muajiriwa atastahiki malipo baada ya kustaafu chini ya mpango wa akiba ya uzeeni ulioanzishwa nje ya Zanzibar na kwamba malipo hayo kwa maoni ya Bodi ni ya kutosha kulingana na hali; na
- (c) muajiriwa si Mzanzibar,

basi itaweza kutoa kwa muajiriwa huyo hati ya kusemeheka (exemption) na baada ya hapo atajaaliwa kuwa si muajiriwa kwa madhumuni ya sheria hii kuhusiana na uajiri wake kwa muajiri huyo kwa kipindi kinachohusika kwa kadri aya (a), (b) na (c) za kifungu hiki zitakavyoendelea kuhusika naye.

SEHEMU YA NANE

KUONDOLEWA KWA MICHANGO.

Kuondolewa
kuidhinishwa na
Bodi.

31. Hakuna kiasi ambacho kimo katika akiba ya mwanachama wa Mfuko kitachoweza kuondolewa isipokuwa kwa idhini ya Bodi na idhini hiyo haitatolewa kabla ya tarehe ya mwanachama huyo kustahiki malipo ya akiba hiyo.

Kuondolewa kwa namna nyenginezo zisizokuwa kwa kifo.

32. Bodi baada ya kufika tarehe ya kustahiki malipo kwa mwanachama kwa njia nyengine isiyokuwa ya kifo na baada ya yeye mwenyewe kuomba au baada ya Kamati iliyochaguliwa chini ya masharti ya sheria ya Wagonjwa wa Akili kuomba kwa niaba yake, itamlipa muombaji kiasi anachostahiki kulipwa kutokana na Mfuko.

Kuondolewa na aliyeteuliwa.

33. Baada ya kifo cha mwanachama ba baada ya maombi yatayofanywa na mtu aliyeteuliwa chini ya masharti ya kifungu cha 25 cha Sheria hii Bodi itamlipa muombaji huyo kiasi cha fedha ambacho mwanachama anastahiki na kama itavyowekwa katika hati ya makubaliano itayofanywa kwa mujibu wa kifungu hicho.

Ushahidi.

34. Maombi yote ya kuondoa mchango yataambatanishwa na ushahidi kama itavyoelezwa, na ushahidi mwengine wowote kama Bodi itavyohitaji zaidi.

Uteuzi.

35. Muajiriwa yeyote au mwanachama wa Mfuko, anaweza kwa kutumia hati itakayofanywa kwa utaratibu utakaoelekezwa, kumteua mtu au watu kupokea malipo kwa niaba yake au kama ni haki ya mtu au watu hao, kutokana na fedha anazostahiki kulipwa kutokana na Mfuko chini ya masharti ya kifungu cha 33 cha Sheria hii wakati wa kifo chake kama hati hiyo itavyoeleza, na muajiriwa yeyote ambaye hatateua mtu huyo ataweza kutakiwa na Bodi kutoa tamko kwa maandishi kwamba hataki kufanya hivyo.

Isipokuwa ndoa itayofungwa na mteuzi huyo baada ya uteuzi huo itaweza kuufanya uteuzi huo uwe batili.

Utaratibu itawapo hakuna mteuliwa au mteuliwa mdogo.

36. (1) Ikiwa, wakati wa kifo cha mwanachama, hakuna mtu aliyeteuliwa chini ya masharti ya kifungu cha 35 cha Sheria hii, basi kiasi cha akiba ya mwanachama kitapelekwa Mahkamani kwa ajili ya

kugawanywa chini ya masharti ya Sheria yoyote inayotumika kwa ajili hiyo.

(2) Iwapo mtu mwingine asiyekuwa **kizuka** ndiye aliyeteuliwa na yuko chini ya umri wa miaka kumi na nane wakati wa kulipwa kwa malipo hayo basi sehemu hiyo ya malipo ya akiba italipwa kwa Mdhadini wa Serikali (Public Trustee) kwa manufaa ya mtu huyo aliyeteuliwa.

Malipo maalum
ya kifo.

37. (1) Endapo kifo cha mwanachama anayestahiki malipo kitatokea baada ya tarehe 1 Januari, 1991, kiasi anachostahiki kitaongezwa kwa kiwango cha kigezo cha juu kama kinavyoweza kuelezwa kwa mujibu wa kijifungu cha (2) cha kifungu hichi na kiwango cha ongezeko hilo kitalipwa kutokana na mapato ya jumla ya Mfuko.

(2) Kiasi kitachoongezwa kwenye akiba ya mwanachama aliyefariki kwa madhumuni ya kijifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki kitahusishwa na muda wa uanachama wa mwanachama na kwa idadi ya kiasi cha mchango uliolipwa kwa niaba yake na kiasi cha akiba kama inavyoweza kuelezwa katika taratibu.

(3) Kiasi cha akiba chini ya kijifungu cha (1) cha kifungu hiki hekitahesabiwa katika kukisia malipo au hasara inayowapaswa kulipwa kwa wanaomtegemea marehemu chini ya masharti ya Sheria ya Fidia ya Wafanyakazi.

SEHEMU YA TISA

UHAULISHAJI KWA JUMUIYA ZA UJENZI.

Matumizi.

38. Masharti ya sehemu hii yatatumika kwa mwanachama waliopata mikopo ya nyumba kutoka jumuiya za ujenzi zitazoidhinishwa na Bodi kwa madhumuni ya Sheria hii.

Kuhaulisha
kutoka akaunti
ya mwanachama
kwenda kwa
jumuiya ya
ujenzi.

39. Bila ya kujali masharti yoyote ya Sheria hii au ya Sheria nyengine yoyote, itakuwa ni halali kwa Bodi baada ya kuombwa na jumuiya ya ujenzi na mwanachama yeyote ambaye masharti ya kifungu cha 38 cha Sheria hii yanahusu, kuhaulisha kwa jumuiya ya ujenzi

kutoka katika akaunti ya mwanachama huyo kiasi cha fedha kisichoziidi kiasi cha akiba ya mwanachama huyo katika siku ya kwanza ya Januari au siku ya kwanza ya Julai ya mwisho inayotangulia tarehe ya maombi hayo.

Maombi ya
Jumuiya ya
Ujenzi kwa
fedha
iliyohaulishwa.

40. Kiasi chochote cha fedha kilichohaulishwa chini ya masharti ya kifungu cha 39 cha sheria hii kitatumiwa na Jumuiya ya Ujenzi kupunguza kiasi cha mkopo uliotolewa na Jumuiya ya Ujenzi kwa mwanachama katika hali ama ya kupunguza muda ambao mkopo huo ungeweza kutolewa au kupunguza kiasi cha viwango vya ulipaji wa deni hilo ambalo, kama si kwa sababu ya kufanywa uhaulishaji, lingepaswa kulipwa na mwanachama kwa Jumuiya ya Ujenzi.

Akiba.

41. Wakati wa kuhaulisha chini ya masharti ya kifungu cha 39 cha Sheria hii, kiwango cha fedha cha akiba ya mwanachama ambaye uhaulishwaji umefanywa kwa kilichohaulishwa lakini mwanachama huyo hatajaaliwa, kuhusiana na uhaulishaji huo tu, kuwa amehaulisha kiasi cha akiba katika maana ya -

- (a) tafsiri ya 'mwanachama anayestahiki' katika kifungu cha 3;
- (b) ibara (c) ya kijifungu cha (2) cha kifungu cha 17; au
- (c) sharti lolote la kifungu cha 21.

Uhaulishaji
kurudi
kwenye Mfuko.

42. Jumuiya ya Ujenzi itaingia katika makubaliano na mtu yeyote ambaye uhaulishaji umefanywa kwa ajili yake chini ya kifungu cha 39 cha Sheria hii ili kuruhusu uwezekano wa kulipa deni lake, ambapo jumuiya hiyo ya ujenzi itazirudisha tena kwenye Mfuko fedha zilizokuwa zimehaulishiwa kwa kiasi kitacholipwa chini ya makubaliano hayo na fedha hizo zitazorudishwa, bila ya kujali masharti mengine ya Sheria hii, zitawekwa bila ya kukatwa, katika akaunti ya mwanachama anayehusika kama kwamba ni mchango uliolipwa kuhusiana na nusu miaka ambayo kiasi hicho hupokewa na Mfuko.

Mpaka wa
Uhaulishaji.

43. Ikiwa uhaulishwaji utakuwa umefanywa kutoka katika akaunti ya mwanachama chini ya kifungu cha 39 cha Sheria hii, hakuna uhaulishaji zaidi utaofanywa tena kutoka katika akaunti ya mwanachama huyo.

SEHEMU YA KUMI

HIFADHI YA FEDHA ZILIZOCHANGWA NA KUONDOLEWA.

44. (1) Bila ya kujali masharti ya Sheria yoyote lakini kwa kuzingatia masharti ya kijifungu cha (2) cha kifungu hiki, hakuna mchango ulioingizwa kwenye Mfuko, wala akiba ya mwanachama wala riba iliyopatikana kutokana na mchango wa akiba hiyo, wala kuondolewa (withdrawals) kulikofanywa kwa ruhusa ya Bodi chini ya vifungu vya 32, 33 na 36 vya sheria hii, wala haki ya mwanachama yeyote aliyonayo chini ya sheria hii, wala haki ya kupata 'annuity' chini ya ibara (b) ya kifungu cha 68 cha sheria hii, vitavyoweza kugawiwa mtu mwingine au kuhaulishwa au kuwa na dhima ya kupigwa tanji, kuwekwa rehani au kukatwa kuhusiana na deni au madai yoyote.

(2) Bila ya kujali masharti ya sheria yoyote fedha zote zitazolipwa kutoka kwenye Mfuko baada ya kifo cha mwanachama zitajaaliwa kuwa zimetolewa na Mfuko kwa ajili ya mtu au watu kama itavyoamuliwa na Mahkama kwa mujibu wa kijifungu cha (1) cha kifungu cha 36.

Ruhusa kwa Bodi
kufanya malipo
nje ya nchi.

45. Bila ya kujali masharti ya sheria nyengine yoyote, Waziri anaweza kuiruhusu Bodi kufanya malipo ya kiasi chochote ambacho kiko tayari kulipwa ama kwa njia ya kuondolewa au malipo ya 'annuity' yanayo-stahiki kulipwa chini ya Sheria hii kwa mwanachama katika nchi yoyote ambayo mwanachama anakaa wakati malipo hayo yatakapokuwa tayari kulipwa.

46. Kwa madhumuni ya sheria yoyote, malipo yoyote kwa ajili ya 'annuity' ambayo yanapaswa kulipwa chini ya amri iliyotolewa kwa mujibu wa

wa ibara (b) ya kifungu cha 68 cha Sheria hii, itajaaaliwa kuwa ni kiasi kilichoondolewa kutoka kwenye Mfuko na itasamehewa kodi au ushuru uliowekwa na Sheria yoyote.

Kufilisika kwa muajiriwa.

47. Kufilisika kwa muajiriwa hakutaathiri kulipwa kwa mchango kutoka katika mshahara wa muajiriwa kwa mujibu wa sheria hii, lakini malipo hayo yataendele kufanywa bila ya kujali masharti ya Sheria yoyote na sehemu hiyo ya mshahara itayolipwa itajaaaliwa kuwa ni sehemu ya mali yake aliyoipata baadae.

Kufilisika kwa mwajiri.

48. (1) Endapo mdhamini yeyote, msuluhishi, wakala au msimamizi au mtu mwingine wa aina hiyo anaeshughulikia mali, shughuli au tirka ya muajiri ambaye ameshindwa kulipa mchango anaopaswa kulipa chini ya sheria, mtu huyo atalipa malipo hayo katika utaratibu utakaowekwa na Bodi kabla hajaigawa mali hiyo au tirka hiyo.

(2) Mdhamini, msimamizi au wakala yeyote kabla ya kuigawa mali iliyo chini ya dhamana yake basi itambidi aipate shahada kutoka kwa Meneja wa Mfuko kuonyesha kuwa malipo yanayostahiki kulipwa chini ya Sheria hii na mtu huyo kutoka katika tirka yoyote iliyochini ya dhamana yake imelipwa.

(3) Ikiwa mali au tirka imegawanywa na mdhamni, msimamizi au wakala bila ya kupata shahada chini ya kijifungu (2) cha kifungu hiki, basi mtu huyo atakuwa na dhima yeye mwenyewe ya kulipa mchango unaotakiwa kulipwa pamoja na ada inayotakiwa kulipwa chini ya kifungu cha 14 cha Sheria hii.

Siri.

49. Bila ya kujali masharti ya Sheria yoyote, Bodi haitalazimika kutoa maelezo kuhusu jambo lolote kuhusu kiasi cha akiba ya mwanachama isipokuwa kwa mwanachama mwenyewe au ikiwa amekufa, kwa aliyeteuliwa, wala kutoa maelezo kuhusu mwanachama au mwajiri isipokuwa kwa idhini ya mwanachama au mwajiri wake.

Isipokuwa hakuna chochote chini ya kifungu hiki kitachoizua Bodi au maafisa wake kutoa ushahidi

kuhusiana na mambo hayo katika kesi yoyote ya jinai.

SEHEMU YA KUMI NA MOJA

MAKOSA, ADHABU NA MASHTAKA.

Makosa na adhabu.

50. (1) Ikiwa mtu yeyote -
- (a) kwa madhumuni yoyote yanayohusiana na sheria hii -
 - (i) kwa kujua atatoa maelezo ya uongo; au
 - (ii) atatoa au atapeleka au kwa kujua atasababisha au kuruhusu kutolewa au kupelekwa waraka wowote ambao anajua kuwa ni wa uongo,
 - (b) atashindwa kulipa kwenye Mfuko katika mwezi wowote kiasi chochote, ambacho chini ya kijifungu (1) cha kifungu cha 14, cha Sheria hii, anawajibika kulipa katika mwezi huo;
 - (c) atamzua afisa au mtumishi yeyote wa Bodi kufanya kazi zake;
 - (d) atashindwa kufuata masharti ya kifungu cha 29 cha Sheria hii;
 - (e) atashindwa kuhaulisha kwenye Mfuko kiasi chochote cha fedha ambacho anatakiwa akihaulishie kwenye Mfuko chini ya masharti ya kijifungu (1) cha kifungu cha 24 cha Sheria hii, kiasi ambacho atatekiwa na kifungu hicho akihaulishe kwa wakati huo;
 - (f) atashindwa kulipa kwa Bodi, katika wakati unachitajika, kiasi chochote cha adhabu ambacho anawajibika kulipa chini ya kifungu cha 15 cha Sheria hii;
 - (g) akiwa Mjumbe au amewahi kuwa mjumbe, afisa au mtumishi wa bodi akawasiliana

moja kwa moja au vyenginevyo au akaeleza kwa mtu yeyote jambo lolote linalohusu shughuli za Bodi ambalo atalijua kutokana na kuwa kwake mjumbe, afisa, mtumishi au wakala isipokuwa kama itakavyohitajika katika kutekeleza kazi zake akiwa kama mjumbe, afisa, mtumishi au wakala wa Bodi au kama itavyoruhusiwa na Bodi;

- (h) atamfanya mjumbe, afisa, mtumishi au wakala wa Bodi au mtu ambaye amewahi kuwa katika kazi hizo, kuwasilisha au kueleza jambo lolote kati ya yaliyoelezwa katika ibara (2) ya kifungu hiki;
- (i) kabla ya siku yake ya kustahiki malipo atampa mtu mwengine, ataiweka dhamana au rahani, ataihaulisha au kukabidhi kwa mtu mwengine mkataba wa bima alioupata chini ya kijifungu (1) cha kifungu 25 cha Sheria hii;
- (j) atashindwa kulipa mchango au ada ambayo anatakiwa kulipa chini ya kifungu cha 48 cha sheria hii;
- (k) atashindwa kuwasilisha, katika wakati uliotajwa, waraka wowote anaotakiwa awasilishe chini ya ibara (c) ya kifungu cha 62 cha sheria hii;

atakuwa mkosa na atakapothibitika hivyo atatozwa faini isiyoziidi shilingi elfu ishirini au kwenda Chuo cha Mafunzo kwa kipindi kisichoziidi mwaka mmoja au yote mawili faini na kifungu.

(2) ikiwa mtu yeyote -

- (a) atafanya mkato kuhusiana na mchango kwa namna yoyote mbali ya ile ya mkato wa mshahara ambao kutokana nao ndio mchango hukisiwa au kufanya mkato katika wakati mwengine wowote zaidi ya wakati ambao mshahara unastahiki kulipwa; na

- (b) atakata kutoka katika mshahara wa mfanyakazi kiasi kikubwa zaidi cha fedha kuliko kile kilichoruhusiwa chini ya Sheria hii; au
- (c) baada ya kufanya mikato atashindwa kulipa kwenye Mfuko katika miezi inayopaswa kulipwa, michango ambayo tayari imeshakatwa kutoka katika mishahara;

atakuwa mkosa na ikithibiti atatozwa faini isiyoziidi shilingi elfu arobaini au kwenda Chuo cha Mafunzo kwa muda usioziidi miaka miwili au yote mawili faini na kifungo.

(3) Bila ya kujali masharti ya sheria nyengine yoyote mashtaka yanaweza kufuguliwa katika muda wa miaka mitatu tokea tarehe ya kufanyika kosa.

taarifa ya mchango uliokuwa haujalipwa.

51. Ikiwa taarifa ya nia ya kufanya hivyo imepelekwa na mwendesha mashtaka kwa mshtakiwa, ushahidi unaweza kutolewa katika mashtaka yoyote chini ya ibara (b) ya kijifungu (1) cha kifungu cha 50 cha Sheria hii, juu ya mchango ambao haujalipwa katika tarehe na kupelekwa hati ya wito kwa mshtakiwa, kuhusiana na waajiriwa wengine, katika mfumo wa shahada iliyotiwa saina na Meneja na, ikiwa mshtakiwa atapatikana na hatia ya kosa hilo, Mahkama iliyomtia hatiani inaweza, bila ya kuathiri haki yoyote chini ya kifungu cha 57 cha Sheria hii, kuamuru mshtakiwa alipe kwenye Mfuko kiasi hicho cha mchango ambacho hakijalipwa, pamoja na mchango wowote ambao haujalipwa hadi siku ya mashtaka ambayo mshtakiwa ameshtakiwa nayo, na masharti ya Sheria ya Adhabu kuhusu faini yatatumika kwa mchango huo au sehemu yake ambao uneamriwa ulipwe.

Madaraka zaidi ya Mahkama.

52. Ikiwa mtu yeyote amepatikana na hatia chini ya masharti ya ibara (3), (f) au (j) za kijifungu cha (1) cha kifungu cha 50 cha sheria hii kashindwa kuhaulisha au kulipa ada yoyote, mahkama iliyomtia hatiani inaweza, bila ya kuathiri masharti

ya kifungu cha 57 cha sheria hii, kuamuru mshtakiwa kulipa kwenye Mfuko kiasi kinachohitajika kuhaulishwa au kulipwa kama ni ada katika namna ile mchango unavyotakiwa ulipwe chini ya masharti ya kifungu cha 51 cha sheria hii.

Chima ya Maofisa wa Mashirika.

53. Endapo kosa chini ya sheria hii limefanywa na Shirika au Jumuiya au umoja wowote wa watu, mtu yeyote ambae wakati wa kutendwa kosa alikuwa Mkurugenzi, Meneja, Katibu au afisa wa aina hiyo au mshirika wa shirika, jumuiya au umoja huo au alikuwa anakimu madaraka hayo basi atajaaliwa kuwa mkosa isipokuwa labda athibitishwe kuwa kosa hilo lilitendwa bila ya ridhaa yake au kushiriki kwake na kwamba alitumia juhudi zote kuzuia kosa hilo, kulingana na namna ya kazi zake katika madaraka hayo.

Malipo ya muajiriwa kwa mkato usio wa halali.

54. Pale ambapo mahkama yoyote itaridhika, itamtia hatiani muajiriwa yeyote ambae amefanya mikato au amejipatia fedha kutoka kwenye fedha za muajiriwa yeyote kwa ajili ya michango yoyote isipokuwa hiyo kuhusiana na masharti ya sheria hii, mahkama inaweza kutoa amri kwa muajiri huyo kumlipa muajiriwa huyo ambae amekatwa kiasi hicho kwa njia isiyo ya halali.

Mashtaka.

55. Mashtaka kwa ajili ya makosa yoyote chini ya sheria hii yanaweza kufunguliwa na Meneja, au na afisa yeyote, mtumishi au wakala wa Bodi alieruhusiwa kimaandishi kwa niaba ya Meneja, na Meneja au afisa yeyote alieruhusiwa, mtumishi au wakala anaweza kuendesha mashtaka bila ya kujali kama yeye ndiye aliyeanzisha shauri hilo au la.

Ushahidi wa nyendo za kesi.

56. Katika kesi yoyote ile iwe ya jinai au madai nyendo za kesi chini ya masharti ya sheria hii, nakala ya kumbukumbu au akaunti ya Mfuko ambayo imetiwa saini na Meneja utakuwa ni ushahidi ulio wazi kwa maandishi hayo yaliyofanywa na madhumuni yake yatakuwa ni kweli, na shahada ambayo itatiwa saini na Meneja kwamba hakuna maandishi yaliyofanywa basi utakuwa ni ushahidi uliowazi.

Kesi za Madai.

57. (1) Michango yote ambayo imelipwa chini ya masharti ya sheria hii, inaweza, bila ya kuathiri malipo mengine yoyote, kupatikana tena kwa Bodi kama ni deni.

(2) Madai yote yanayohusiana na madeni ya mchango wowote yanaweza, bila ya kujali chochote katika Sheria nyengine yoyote vyenginevyo, yanaweza kufunguliwa wakati wowote katika kipindi cha miaka sita kuanzia tarehe ambayo mchango huo ulitolewa.

(3) Madai yanayohusiana na madeni ya michango yanaweza yakafunguliwa na Meneja, au na afisa yeyote, mtumishi au wakala wa Bodi aliyeruhusiwa kimaandishi kwa niaba ya Meneja. Meneja au afisa, mtumishi au wakala yeyote aliyeruhusiwa anaweza akaendesha madai hayo.

(4) Katika kifungu hiki neno "mchango" litajaliwa kujumuisha malipo ya ziada ya masharti ya kifungu cha 15 cha sheria hii.

Upoteaji wa maslahi kutokana na makosa ya muajiri.

58. Ikiwa, kama itatokezea kwa muajiri kukosa kulipa mchango wowote kwa kipindi ambacho mchango huo ulistahiki maslahi yoyote chini ya masharti ya sheria hii ambayo yangukuwa yalipwe kwa mtu yeyote, ikiwa malipo hayo hayakulipwa, muajiri huyo, kama atapatikana na hatia katika mahkama yoyote kwa kushindwa kulipa mchango huo wakati uliostahiki, atakuwa ni mkosa na atalipa kwenye Mfuko kiasi cha maslahi ambayo yangelipwa kutokana na mchango ambao ungelipwa kwa wakati.

Madai.

59. Kiasi chochote ambacho muajiri atakuwa na jukumu la kulipa chini ya masharti ya kifungu cha 58 cha sheria hii, yatalipwa kwa Bodi kama ni deni na madai ya madeni hayo yanaweza yakafunguliwa na mtu yeyote aliyeruhusiwa kufungua madai chini ya masharti ya kifungu cha (3) cha kifungu cha 57 cha sheria hii.

hi ya kiasi
chorudishwa
Bodi.

60. Kiasi chochote kilichorudishwa kwa Bodi chini ya masharti ya kifungu cha 58 au 51 cha Sheria hii, yatalipwa na Bodi kwa mtu au watu ambao walistahiki, lakini kutokana na makosa ambayo muajiri ametiwa hatiani, anastahiki kupokea kiasi hicho chini ya masharti yoyote ya sheria hii, na kwa ajili ya kifungu cha 44 cha sheria hii malipo hayo yatajaaliwa kuwa yamelipwa kutoka kwa Mfuko.

ada itayo-
wa na Meneja.

61. Kwa madai yaliyofunguliwa chini ya masharti ya kifungu cha 59 cha Sheria hii, shahada yenye sahihi ya Meneja kwa kiasi cha maslahi ambayo yangelipwa kutokana na kosa ambalo muajiri ametiwa hatiani bila ya kosa hilo itakuwa ni ushahidi ulio wazi kuhusiana na deni hilo.

SEHEMU YA KUMI NA MBILI

UWEZO WA WAKAGUZI NA MAOFISA WA MFUKO.

co wa
aguzi.

62. Mkaguzi yeyote aliyeteuliwa chini ya masharti ya kijifungu cha (3) cha kifungu cha 6 cha sheria hii anaweza kwa wakati unaokubalika;

- (a) kuingia kwenye eneo au pahala popote ambapo watu wanaaminika kuwa ni waajiriwa;
- (b) kufanya uchunguzi kama itavyoonekana muhimu, wa kuona kwamba masharti ya sheria hii yanafuatwa ipasavyo katika maeneo hayo;
- (c) kupata nyaraka zozote ambazo muajiri anatakiwa kuziweka chini ya masharti ya sheria hii au chini ya sheria ya uajiri au nyaraka zozote zinazohusiana na mkataba au masharti ya utumishi yaliopo kati ya muajiri na muajiriwa au waajiriwa wake, na kwa ajili hii, hati ya maandishi inaweza kutumwa kwa muajiri ama kuhusiana na masharti ya kijifungu cha (6) cha kifungu

cha 2 cha Sheria ya Ufafanuzi au kwa hali yoyote kwa kuifanyia usajili kwa njia ya posta kwa kutumia anuani ya muajiri, kwa madhumuni ya kumfanyia ukaguzi muajiri huyo kwa tarehe ambayo imeelezwa katika hati hiyo, isipokuwa kwamba tarehe iliyeleleza isiwe chini ya siku ishirini na moja kuanzia siku iliyotumwa hati hiyo na hati hiyo itajaaliwa kuwa imetumwa kwa muajiri wakati itapokuwa imefika kwenye posta ya karibu.

- (d) kumchunguza, ama akiwa peke yake au mbele ya mtu mwingine yeyote, kwa ajili ya jambo lolote chini ya sheria hii ambalo kuhusiana nalo anaweza kuhitaji habari, mtu yeyote ambae ana sababu ya kuamini kwamba anaweza kutoa habari za kuaminika kuhusiana na jambo linalofanyiwa uchunguzi na kutaka mtu huyo ahojiwe, na kwa madhumuni ya uchunguzi huo mtu huyo anaweza kuitwa na kutakiwa kuhudhuria kwa wakati na mahali ambapo pameelezwa katika wito huo.

Uwezo wa
naofisa wa
Mfuko.

63. Mkaguzi, au mtu yeyote alieteuliwa chini ya masharti ya kifungu cha 6 cha Sheria hii na ambae ameruhusiwa kimaandishi na Meneja, anaweza kufanya uchunguzi kama itavyoonekana muhimu, kwa kupata ukweli wa hoja yoyote iliyofanywa kwa madhumuni ya kujua tarehe inayostahiki kwa mwanachama wa Mfuko na anaweza kwa madhumuni hayo -

- (a) kumchunguza aidha akiwa peke yake au mbele ya mtu mwingine yeyote, kwa ajili ya jambo lolote chini ya Sheria hii ambalo kuhusiana nalo anaweza kuhitaji habari, mtu yeyote ambae ana sababu za kuamini kwamba anaweza kutoa habari za kuaminika kuhusiana na jambo linalofanyiwa uchunguzi, na kutaka mtu huyo ahojiwe, kwa madhumuni ya uchunguzi huo mtu

huyo anaweza kuitwa na kutakiwa kuhudhuria kwa wakati na pahala ambapo pameelezwa katika wito huo;

- (b) kumtaka mtu yeyote ambae ametoa hoja hiyo kutia saina kwamba maelezo hayo ni ya kweli.

SEMEMU YA KUMI NA TATU

MAELEZO YA JUMLA

Maombi ya mkopo kwa mwanachama.

64. Mwanachama wa Mfuko anaweza kupeleka maombi yake kwa Bodi kwa ajili ya kupatiwa mkopo kutoka kwenye Mfuko kwa madhumuni ya kununua mali inayoweza na isiyoweza kuhamishika.

Isipokuwa kwamba, pale ambapo mkopo umeombwa na kuthibitishwa, mkopo huo utatolewa sio zaidi ya mwezi mmoja kuanzia tarehe ambayo maombi hayo yalifanywa.

Malipo yafanywe kwa kipindi cha miezi sita.

65. Malipo yoyote yanayofanywa kwa ajili ya mwanachama wa Mfuko au kuto kana na kifo cha mwanachama huyo, kwa wanaomtegemea wakati malipo hayo yanapokua tayari, yatalipwa ndani ya kipindi cha miezi sita kuanzia tarehe ambapo malipo hayo yameidhinishwa au tarehe ambayo kifo kimetokea.

Makosa na adhabu.

66. (1) Afisa yeyote ambae atachelewesha malipo yoyote yaliyofanywa chini ya kifungu cha 65 cha sheria hii atakuwa ametenda kosa.

(2) Kosa ambalo limetendwa na afisa litajaaliwa kama kwamba limetendwa na Mfuko, na Mfuko utatiwa hatiani kwa kutozwa faini ya asilimia 10 ya kiasi ambacho mwanachama anaestahiki au wanaomtegemea kacheleweshwa kwa kila mwezi ambao utacheleweshwa au sehemu ya mwezi huo kulipwa kwa mwanachama au wanaomtegemea kutokana na fedha za Mfuko.

(3) Afisa yeyote ambae atatenda kosa chini ya kifungu hiki kesi yake itashughulikiwa chini ya masharti ya Sheria ya Usalama Kazini.

SEHEMU YA KUMI NA NNE.

Kanuni.

67. Waziri anaweza kutunga Kanuni kwa madhumuni yoyote ambayo kanuni zinaweza kutungwa chini ya masharti ya Sheria hii na kwa ajili ya kuelezea chochote ambacho kinaweza kuelezewa na vyenginevyo kwa ajili ya kuendeleza Sheria hii kutumika, bali bila ya kuathiri maelezo ya jumla, anaweza kufanya kanuni kwa ajili ya mambo yafuatayo -

- (a) kuweka utaratibu wa usajili wa waajiri na waajiriwa kabla ya kuanza kutumika masharti yoyote ya Sheria hii;
- (b) kuweka taratibu za kulipa na ukusanyaji wa michango na mambo mengine yahasikanayo na hayo;
- (c) kuhughulikia kiasi ambacho hakikudaiwa, hakikulipwa au kimebakia katika Mfuko;
- (d) kuelezea -
 - (i) marejesho ya michango chini ya masharti ya sheria hii, au sehemu yoyote ya michango hiyo, iliyolipwa kimakosa;
 - (ii) malipo ya michango chini ya masharti ya sheria hii, au sehemu yoyote ya michango hiyo, iliyowachwa kulipwa kimakosa.
- (e) kuweka taratibu na masharti ya uwekaji na utunzaji wa vitabu vya mahesabu na kumbukumbu za waajiri;
- (f) kuweka taratibu na masharti ya uteuzi wa Bodi ya madaktari kwa ajili ya ibara (c)

ya tafsiri ya "tarehe inayostahiki" kwenye kifungu cha 3 cha Sheria hii na kwa ajili ya madhumuni kama itavyoelezwa;

- (g) kueleza masharti na taratibu za kutoa fedha kutoka kwenye Mfuko;
- (h) kuelezea namna ushahidi utavyotolewa na mtu atakaetoa, afisa au aliemruhusu ambaye kwake ushahidi utatolewa kwa ajili ya kifungu cha 34 cha sheria hii;
- (i) kuelezea taratibu za kufuatwa wakati michango inapolipwa na muajiri kwenye Mfuko;
- (j) kuelezea namna na wakati hati yoyote itatolewa na muajiriwa kwa muajiri wake chini ya masharti ya ibara (c) ya kijifungu cha (3) cha kifungu cha 14 cha Sheria hii;
- (k) kuelezea taratibu za kufuatwa wakati m-chango wowote wa hiari unapolipwa kwenye Mfuko;
- (l) kuelezea marejesho yatayofanywa na waaajiri, na fomu za madaftari ambayo yatatumika katika kutekeleza masharti ya Sheria hii;
- (m) kuelezea kiasi na namna ya malipo na muda wa malipo yoyote ambayo yatalipwa chini ya masharti ya ibara (b) ya kifungu cha 68 cha sheria hii.

Kusamehe malipo ya miaka.

68. Waziri anaweza, kwa uwezo mwengine wowote alionao chini ya masharti ya Sheria hii, baada ya kuwasiliana na Bodi;

- (a) kwa kutoa toleo, kumruhusu mtu yeyote au kikundi cha watu kutofungika na masharti yoyote ya Sheria hii;
- (b) kuelezea kwa toleo kwamba, bila ya kujali masharti ya vifungu vya 32, 33, 36

na 37 vya Sheria hii, mtu yeyote, au kikundi cha watu, wanachusika chini ya masharti ya vifungu vyote kupokea kiasi chochote au sehemu ya kiasi cha akiba ya mwanachama katika Mfuko, anaweza kupokea, badala ya watu wa sehemu yoyote wanayostahiki nayo, fedha kwa kiwango hicho au sehemu yake.

Makubaliano
mengine.

69. (1) Waziri baada ya kushauriana na Bodi, anaweza kuingia katika makubaliano ya kubadilishana na Serikali ya nchi nyengine yoyote ambayo mfuko wa aina hii ya Mfuko umeanzishwa na makubaliano hayo yanaweza kuelezwa, miongoni mwa mambo mengine kama -

- (a) muda wote wa kazi kwa muajiri katika nchi hiyo utajaaliwa kama kwamba ni muda wa kazi kwa muajiri wa Zanzibar kwa ajili ya tafsiri ya "muajiriwa" katika kifungu cha 3 cha Sheria hii; na
- (b) kwa kufuata masharti ambayo yatawekwa katika mkataba wa makubaliano kuhusiana na madai ya malipo ya mwanachama wa Mfuko ambae anamfanyia kazi mwajiri wa nchi hiyo, malipo anayostahiki yanaweza kuhalishwa kwenye mfuko huo; na pia malipo au madai ya mtu yeyote aliyekua nje ambae atakua mwanachama wa Mfuko yanaweza kuhalishwa katika akiba yake ya Mfuko, na iwapo katika mkataba wa makubaliano yaliyofikiwa ambayo yatatoa tafsiri ya neno "mwajiriwa" iliyopo katika kifungu cha 3 cha sheria hii, na itajaaliwa kufasiriwa kwa mujibu wa hali, hata hivyo hakuna mtu ataetakiwa kuchangia katika Mfuko katika kipindi ambacho hakuwa akifanya kazi katika Zanzibar na mwajiri wake atatakiwa kuchangia kuhusiana na mwajiriwa katika kipindi hichi cha kuhaulishwa na Bodi kwa madai kutoka au kuingia katika Mfuko kwa namna itavyoruhusiwa.

(2) Mkataba wowote wa makubaliano uliofikiwa chini ya masharti ya kifungu cha (1) cha kifungu hiki yatachapishwa katika Gazeti Rasmi na yataanza kutumika tarehe ambayo itatangazwa baadae ambayo imeainishwa katika makubaliano au tarehe ya kuchapishwa kwa Gazeti hilo.

JADWELI YA KWANZA

WALIOSAMEHEKA

(CHINI YA KIFUNGU CHA 3)

1. Mtumishi yeyote wa nyumbani au mtoto kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Kazi.
2. Mfanyakazi yeyote wa nje kama ilivyotafsiriwa na Sheria ya Fidia ya Wafanyakazi.
3. Mtu yeyote aliezuiliwa katika gereza lolote, skuli ya manunda, hospitali za wagonjwa wa akili au kwenye nyumba za wenye maradhi ya ukoma.
4. Mtu yeyote ambae ni mwanachama wa Mfuko wa Akiba ulioanzishwa na masharti ya sheria nyengine yoyote.
5. Mtu yeyote ambae amejiunga tena na Mfuko chini ya masharti ya ibara (i) ya maelezo ya kifungu cha (1) cha kifungu cha 21 na kuondoa kiasi cha akiba yake kwenye Mfuko.

JADWELI YA PILI

KIMA CHA MCHANGO

(CHINI YA KIFUNGU CHA 14)

Mchango wa mwezi kwa muajiri chini ya masharti ya kifungu (1) cha kifungu cha 14 utakuwa ni asilimia kumi na taná ya kima cha mshahara wa muajiriwa kwa mwezi wa nyuma, na kiasi kinachoweza kujilipa muajiri chini ya masharti ya kifungu cha (2) cha kifungu hicho

kutoka kwenye mshahara wa muajiriwa kwa mwezi wa nyuma kitakuwa ni asilimia tano ya mshahara wa muajiriwa wa mwezi huo.

Isipokuwa kwamba, iwapo katika mwezi wowote kima cha mshahara kilicholipwa kwa muajiriwa hakizidi senti thelathini kwa sasa, hakuna kiasi kitacholipwa na muajiriwa kutoka kwenye mshahara wa muajiriwa kwa mwezi huo.

Imepitishwa na Baraza la Wawakilishi tarehe 30 Machi, 1990.

KHAMIS JUMA CHANDE
KATIBU

BARAZA LA WAWAKILISHI LA ZANZIBAR.